# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*

*Zanzibar*
*14 Machi, 2024*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**UKOMBOZI WA MWANAMKE UNAPASWA KUWA KIPAUMBELE – SAMIA**

Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa taasisi za kiserikali na sekta binafsi kufanya jitihada za kuhakikisha wanawake wanapata nafasi na kusikika kwenye maamuzi mbalimbali nchini.

Rais Samia amesema hayo leo kwenye mkutano wa wanawake walio katika sekta ya fedha uliofanyika ukumbi wa hoteli ya Kwanza iliyopo Kizimkazi.

Aidha, Rais Samia amesema ushiriki wa wanawake kwenye ngazi za maamuzi ni suala jumuishi na endelevu hivyo halipaswi kuchukuliwa kama la kimapinduzi au la serikali pekee.

Rais Samia amebainisha kuwa lengo ni kuhakikisha masuala yanayowahusu wanawake ambayo wafanya maamuzi wengine wanaweza wasiwe na uelewa nayo yanapata nafasi kwenye meza ya maamuzi.

Hali kadhalika, Rais Samia amesema pamoja na kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye ngazi za maamuzi lazima pia kuweka nguvu kubwa katika kuwainua wanawake kiuchumi.

Kwa upande mwingine, Rais Samia amewataka wanawake kujipanga na kufikia malengo yao kwa vitendo.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu